Jarida la

# SAUTI YA JIJI

DAR ES SALAAM

Toleo na/ Dcc/ 014



# Waziri Mkuu atoa maagizo kwa Maafisa Habari nchini

- Awataka kuzingatia weledi
- Asisitiza uwajibikaji




## MAADHIMISHO SIKU YA WANAWAKE DSM YAFANA - RC MAKALLA

## DC Ilala Ashiriki zoezi la usafi

- Aahidi kusimamia Mazingira
- Barabara ya Lumumba chini ya Uangalizi maalum



Lipia ya Leseni ya Biashara ,ushuru wa maegesho kwa kutumia mfumo wa Tausi

*kwa Taarifa zaidi tembelea Tovuti yetu. www.dcc.go.tz*



# Waziri Mkuu awataka Maafisa Habari Nchini kutekeleza wajibu wao

Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa amewataka Maafisa habari kutumia vyema elimu na uzoefu walionao kutoa taarifa sahihi kwa wakati hasa kwa Serikali na Viongozi wetu huku akiwataka watekeleza wajibu wao katika kutimiza majukumu yao ya kutoa taarifa kwa Wananchi.
Waziri Majaliwa ameyasema hayo leo Mchi 27, 2023 wakati akifungua Kikao kazi cha 18 cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serekalia kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere International Conventional Centre (JNICC) Jijini Dar es Salaam.
Aidha Waziri Majaliwa ametoa wito kwa Maafisa Habari kuongeza ubunifu ili kusukuma agenda za Serikali kuwafikia wananchi. "Ndugu wanahabari hakikisheni mnafanya kazi ya kutoa habari sahihi kwa ukamilifu na kwa wakati ili wananchi waweze kufikiwa na habari hizo kwani Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anatambua mchango mkubwa mnaoufanya katika kuchochea miradi mbalimbali na hatowaangusha atashirikiana na nyinyi bega kwa bega kuhakikisha sekta hii ya habari inasimama imara.
Vilevile Waziri Majaliwa ameendelea kusema "Ni matumaini yangu mtatoa taarifa za utekelezaji wa miradi kwa wananchi hivyo niwahakikishie kwamba Serikali inatambua mchango wenu na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan anatarajia baada ya kikao hichi tasnia hii itaenda kufanya mabadiliko makubwa katika utoaji wa taarifa mbalimbali za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya nchi yetu kwa wananchi."
Sambamba na Ufunguzi huo Mhe. Waziri Mkuu aliweza kupokea tuzo ya heshima kwaajili ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wake katika kukuza tasnia ya habari nchini pia aliweza kuzindua jarida la 'Nchi yetu' linaloeleza mafanikio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha uongozi wa miaka miwiliya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Kwa upande wake Waziri wa Habari,mawasiliano na Teknolojia ya habari Mhe. Nape Nauye ameeleza kuwa "Nashukuru sana Jitihada za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutambua umuhimu wa sekta ya habari pamoja na kudumisha Demokrasia nchini kwani aliweza kuhudhuria mkutano wa hadhara kwa Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo hivyo ni imani yangu kikao hichi kitawajengea uwezo katika kusukuma maendeleo ya nchi yetu."
Sambamba na hilo Mhe. Nnauye amekitaka Chama cha TAGCO kutekeleza majukumu yake bila kujitegemea hivyo baada ya kikao hichi Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itasimamia na kuratibu mambo yote ya maafisa habari, mawasiliano na uhusiano Serekalini.
Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Bw. Selestine Gervas Kakele amesema "Katika Kikao kazi hichi cha 18 Kutakua na mada mbalimbali zitakazo tolewa kwa Maafisa habari wetu ambapo kutakua na mada ya kujifunza jinsi ya kuhariri habari, mada kuhusu uboreshaji na utunzaji wa Mazingira, Wajibu wa Maafisa habari katika uchaguzi wa viongozi wa Nchi yetu."
Sambamba na hilo Bw. Kakele Ameeendelea kusema baada ya kikao hichi matarajio yetu ni kuwa maafisa habari hawa watakua wamejengewa uwezo wa kutoa taarifa zinazolinda taasisi zao, maarifa ya kupata taarifa Sahihi kwa wakati kwa vyanzo husika, kutoa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wananchi pamoja na kuwahoji wananchi

# JUKWAA LA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHIMI WILAYA YA ILALA LATAPA MWENYEKITI MPYA



Wanachama wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Wilaya ya Ilala wamemchagua Bi. Rehema Sanga kuwa Mwenyekiti wa Jukwaa hilo huku Makamu Mwenyekiti akichaguliwa Bi. Lulu Nyapili katika Uchaguzi uliofanyika katika Ukumbi wa mikutano wa Arnatouglo.

Aidha, wanajukwaa hao wamemchagua Bi. Lucy Mbwale kuwa Katibu wa Jukwaa na Rukia Mshuza kuwa Katibu Msaidizi huku Bi. Zainabu Heggah Kutoka Kata akishinda nafasi ya Muweka Hazina.
Akizungumza baada ya Uchaguzi huo, Mwenyekiti wa Jukwaa hilo Bi. Rehema Sanga, amewashuru wajumbe Kwa imani waliyompa na kuahidi kuwatumikia Kwa moyo wote

“Nimekua na ndoto ya Kuwatumikia Wanawake wenzangu hivyo kupitia nafasi hii nitashirikiana na Wenzangu kuanzisha miradi ili kukuza uchumi wetu wanajukwaa” alisema Bi. Sanga

Kwa Upande wake Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Bi. Francisca Makoye amewapongeza Wanajukwaa kwa kufanikisha uchaguzi na kuahidi kuendelea kuwapa Ushirikiano kwa kutekeleza takwa la kisheria la kuwezesha Makundi ya Wanawake kujikwamua kiuchumi kupitia Mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kutoka Mapato ya ndani ya Halmashauri.



Mwenyekiti Mpya wa Jukwaa la kuwezesha wanawake Kiuchumi Bi Rehema sanga

# Bilioni 2.9 Yatolewa kwa wanufaika wa mikopo ya Asilimia 10% ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam




Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii leo Machi 7, 2023 wamefanya hafla ya kukabidhi mikopo kwa vikundi vya wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu ambapo shilingi bilioni 2.9 zimetolewa ikiwa ni fedha kwa ajili mkopo wa asilimia 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa wanufaika hao.

Akizungumza katika hafla iyo DC Mpogolo amesema "Niwaombe sana wanufaika wa mikopo hii muwe na nidhamu ya marejesho ya fedha hizi kwani Mheshimiwa Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan anatambua uwepo wa makundi haya ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na ndio maana katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mheshimiwa Rais ameweza kuelekeza Halmashauri zote zitoe mikopo kwa makundi haya pia ameruhusu Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kutoka mkopo hadi bilioni 2.9 lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanajiajiri wenyewe na wanajikwamua kiuchumi hivyo niwaombe mkipewa mikopo hii mhakikishe mnarejesha fedha hizo kwa wakati ili wengine waweze kupata kwani wahitaji bado ni wengi."

Sambamba na hilo Mhe.Mpogolo ameeleza kuwa japo vikundi hivi vinapata mikopo na vimejiajiri ila Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na timu yake waweze kuwatafutia masoko wananchi hawa wanaopokea mikopo ya asilimia 10%hivyo amewaombaa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia idara yake ya maendeleo ya Jamii wanaandaa Soko angalau mara mbili kwa mwaka kwaajili ya kusaidia vikundi hivi.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Eng. Amani Mafuru ameeleza kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii inaendelea kutekeleza jukumu la kutenga na kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ikiwa ni fedha kutoka mapato ya ndani ambapo hadi kufikia Juni 2022 takribani shilingi bilion 23.4 ziliweza kutolewa kwa vikundi 1963 vyenye wanufaika elfu 19.8 ambapo shilingi bilioni 19.9 zikiwa ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri huku shilingi bilioni 5.5 zikiwa ni fedha kutoka katika marejesho ya mikopo hiyo.

Akiendelea kutoa taarifa katika hafla hiyo Eng.Mafuru amesema "kuanzia mwezi Julai 2023 Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeanza kutoa mikopo kwa




kuzingatia mfumo wa kielektronic (Ten Percent Loan Management Infomation System) ulioanzishwa na Serikali kuu kwa lengo la kurahisisha usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo hiyo hivyo kupitia mfumo huu Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweza kusajili takribani vikundi 1870 na imepokea jumla ya maombi ya mkopo kwa vikundi 458 vyenye thamani ya shilingi bilioni 33 ambapo baada ya uhakiki Halmashauri imepanga kutoa mikopo hiyo kwa awamu kupitia fedha za marejesho kutoka kwenye mikopo ya vikundi vingine."
Sambamba na hilo Eng. Mafuru ameeleza kuwa "lkiwa ni awamu ya Kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inatoa mikopo kwa vikundi 76 vyenye wanavikundi 360 ambapo vikundi 27 vinatoka Jimbo la Ilala, vikundi 23 kutoka Jimbo la Ukonga huku vikundi 26 vikitoka Jimbo la Segerea ambapo vikundi hivyo vitapewa mkopo kulingana na mgawanyo wa asilimia 4% kwa Wanawake, asilimia 4% kwa vijana na asilimia 2% kwa watu wenye ulemavu kwani vikundi hivi vimeshapata mafunzo na kusaini mikataba tayari kwa kuwekewa hela hizo."
Akitoa Shukurani zake za dhati kwa niaba ys wanavikundi wengine waliopokea hundi za mfano Deogratius Davidi kutoka kikundi cha Good Hope ameweza kumshukuru Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan kwa utoaji wa mikopo bila kusahau juhudi za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kuweza kuandaa mafunzo na pia kutoa ushauri kwa vikundi hivyo kwani hii imeweza kupunguza wimbi la ukosekanaji wa ajira kwa vijana hivyo wameahidi kuzitumia fedha hizo kwa umakini na kurejesha marejesho kwa wakati ili wengine waweze kunufaika.



# VIKUNDI VYA WAJASILIAMALI ILALA VYAPEWA MAFUNZO YA UMUHIMU NA MATUMIZI YA MSIMBOMILIA ( BARCODE )




Tarehe Iliyowekwa: March 9th, 2023

Mkuu wa Wilaya Ilala Mhe. Edward Mpogolo amewahakikisha Wajasiriamali Wilaya ya Ilala kuwapa ushirikiano pale wanapohitaji ili kukuza Masoko ya Wajasiriamali hao.

Amebainisha hayo leo Machi 09, 2023 wakati akifungua Semina ya Mpango wa Mafunzo ya Ujasiriamali kwa ngazi ya Halmashauri iliyofanyika katika Ukumbi wa Arnatoglou Jijini Dar es Salaam, Semina hiyo iliwezeshwa na taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo TRA, TIRDO, TCCIA, BRELLA, TANTRADE na TBS.

Akifungua mafunzo hayo Mhe.Mpogolo Amesema “Mafunzo haya ni adhimu sana kwa wajasiriamali kwani suku hii ya leo watapata mafunzo haya yenye lengo la kuwajengea uwezo wa kutafuta Masoko baada ya kuweka bidhaa zao Barcodes ambayo itawasaidia kuuza bidhaa hizo kwenye masoko rasmi hivyo niwaombe Wajasiriamali msikilize kwa makini na muende mkaishi haya yote mnayoelekezwa.”

Kwa upande mwingine Mhe. Mpogolo aliweza kuzindua kampeni ya GS1 Tanzania Barcode day itakayoanza June 15-19, 2023 yenye kauli mbiu isemayo ‘GS1Tanzania beyond Barcode’ ambapo aliweza kuwasisitiza wajasiriamali kujitokeza kwa wingi, “Ili kuwakomboa kina mama lazima kina mama muungane na mimi niwahakikishieni kwenye hiyo kampeni ya Kata kwa Kata nitakuwepo kwani tutafanya kwa niaba ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan ambaye nia yake ni kuwakomboa wananchi kiuchumi hususani Wanawake hivyo nawapongeza GS1 na timu nzima kwa kampeni hizi naamini kila Mjasiriamali wa Wilaya ya Ilala atanufaika na fursa hii.”

Naye Mwakilishi wa Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Jiji la Dar es Salam Bi. Tabu Shaibu awashukuru GS1 kuandaa semina ya mafunzo kwa Wajasiriamali ambayo itawasaidia kupata uelewa jinsi ya kuboresha bidhaa zao ili ziwe na viwango na ubora na kuweza kukidhi Soko la ushindani ambapo zitaweza kukuwa na kufikia Soko la kimataifa.

Aidha, kwa upande wake mwakilishi wa Kaimu Mkurugenzi Halmshauri ya Jiji la Dar es Salaam Bi. Tabu Shaibu amemuhakikishia Mkuu wa Wilya kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia



Kitengo chake cha Maendeleo ya Jamii iko tayari kuyafanyia kazi yale yote yaliyoelekezwa kwenye semina hiyo ili kuinua Wajasiriamali hao.Pia awataka Wajasiriamali kusikiliza kwa makini semina hiyo ya mafunzo ili kutoka na uelewa jinsi gani ya kuboresha bidhaa zao.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa GS1 Bi. Kange Ameeleza kuwa “Baada ya Wajasiriamali kuonekana wanazalisha bidhaa bora lakini hazina msimbomilia(BARCODE) Ofisi ya Rais TAMISEMI wakaona ni vyema kutoa kibali kwa Taasisi ya GS1 ambao ndio hutengeneza Barcodes kuandaa mafunzo katika kila Halmashauri nchini ya kuwafundisha Wajasiriamali umuhimu wa Barcodes ambapo kila Halmshauri iliweza kuingia makubaliano ya mafunzo hayo kwa kuchangia Shilingi Milioni 5 zakuwezesha mafunzo hayo hivyo mafunzo haya ya kuwajengea uwezo Wajasiriamali juu ya umuhimu na matumizi ya msimbomilia (BARCODES) yameanza kufanyika leo kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambapo vikundi Vitano (5) Vitaweza kuchaguliwa.”

Sambamba na hilo Bi. Kange ameeleza kuwa baada ya mafunzo wataweza kuwasaidia wafanyabiashara kutafuta masoko kwani kuna masoko Canada na Marekani ila masoko haya yatahudhuriwa na vikundi ambavyo vitaweza kukidhi vigezo na pia vitakavyotengeneza bidhaa bora na zenye viwango

Aidha Bi.Kange ameendelea kusema “Sisi kama wajasiriamali tuhakikishe tunatengeneza bidhaa kwa kiwango na pia tunaweka mifumo kupitia Maafisa Maendeleo wa Halmashauri ya Jijj la Dar es Salaam huku tukipanga kiwango cha pamoja cha kuuza bidhaa zetu hivyo niwasisitize mtengeneze kurasa za mitandao ya kijamii kwaajili ya kutafuta masoko rasmi.

# RC Makalla Aongoza Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Mkoa wa Dar es Salaam




Tarehe Iliyowekwa: March 8th, 2023

Kila Tarehe 08 Machi Taifa linaadhimisha siku ya Wanawake Duniani ambapo Leo Machi 08, 2023 maadhimisho hayo katika Mkoa wa Dar es Salaam yameweza kuadhimishwa katika viwanja Vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam huku mgeni rasmi akiwa ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla.

Katika maadhimisho hayo yenye kauli mbiu isemayo "UBUNIFU NA MABADILIKO YA TEKNOLOJIA NI CHACHU KATIKA KULETA USAWA WA KIJINSIA" yameweza kubeba sura ya Kongamano la Wanawake na Fursa za Kiuchumi, yaliwapa nafasi kina mama na vikundi mbalimbali vya ujasiriamali kushiriki, kuonyesha bidhaa zao, na kuuza bidhaa hizo.

Akiongea katika maadhimisho hayo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe.Amos Makalla amesema "Kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamuhuri ya Muunguno wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuwawezesha Wanawake kiuchumi kupitia mikopo ya Halmashauri kwani Billioni 13.9 zimeweza kutolewa kwaaajili ya kusaidia vikundi vya Wanawake,Vijana pamoja na watu wenye ulemavu ikiwa bilioni 6.1 wamepewa Wanawake huku bilioni 5.9 zikielekezwa katika vikundi vya Vijana na bilioni 1.8 zikielekezwa katika vikundi vya watu wenye ulemavu ambapo takribani vikundi 1243 vimeweza kunufaika na mikopo hiyo ikiwa vikundi 69 ni vya wanawake vukundi 428 ni za vijana na vikundi 126 vikiwa ni vya watu wenye ulemavu hivyo natoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam mjitokeze kwa wingi kunufaika na fursa hii ya mkopo wa asilimia 10%ya mapato ya ndani ya Halmashauri ili muweze kujikwamua kiuchumi pia kwa wale ambao mshapata mikopo hiyo mhakikishe mnarejesha fedha hizo kwa wakati ili wengine nao waweze kupata mkopo."

Aidha Mhe Makalla ameendelea kusema "Mimi kama kiongozi wa Serikali nimeona niwaoneshe kwamba ninaheshimu Wanawake na kuthamini juhudi zao wanazozifanya kuhusu usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ambapo leo hii duniani kote wanaadhimisha siku ya Wanawake kama sisi Tanzania ambapo kitaifa hufanyika kila baada ya Miaka mitano, na Kila Mwaka kila Mkoa hufanya katika Mkoa wake lengo likiwa kuwawezesha Wanawake kujikwamua Kiuchumi, kielimu,kiafya pamoja na kuwawezesha wajasiriamali."

Sambamba na hilo Mhe. Makalla ameweza kuzishukuru Taasisi, Mashirika na Makampuni binafsi ambayo yameweza kuwaruhusu wanawake kuweza kuungana na wanawake wengine siku hii ya leo niwaase Wanawake kuwa wamoja katika kutetea haki zenu na Taifa letu kwa ujumla na ndio maana hata mimi nimeheshimu siku hii nakuweza kuungana na ninyi.

Vilevile Mhe.Makalla aliweza kukagua mabanda ya wajasiriamali kutoka Halmashauri zote zaMkoa wa Dar es Salaam ambao ni wanufaika wa Mkopo wa asilimia 10% za mapato ya ndani ya Halmashauri ambapo aliweza kujionea bidhaa mbalimbali wanazotengeneza wanawake wajasiriamali huku akitoa rai kwa wanawake kuhakikisha wanapata mafunzo ili waweze kupata Masoko ya ndani na nje, " nitoe wito kwa wanawake wathibiti ubora wote kuwatia wanawake wengine moyo

tusiwakatishe tamaa ili waweze kukua kiuchumi pia nitoe wito kwa Jamii kujenga tabia ya kununua bidhaa zinazozalishwa kwa mikono ya wajasiriamali wenzetu na pia wajasiriamali mhakikishe mnatengeneza bidhaa zinazokidhi ubora na viwango ili muweze kupata Masoko ndani na nje ya nchi." Amesisitiza Mhe. Makalla.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo ambaye ni mwenyeji katika maadhimisho haya yaliyofanyika katika Wilaya ya Ilala amesema "Kwa niaba ya Wakuu wenzangu wa Wilaya Nyingine nipende kuwapongeza wamama wa Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam ambao wameweza kujiajiri kupitia mkopo wa Asilimia 10% za mapato ya ndani ambapo hii leo wameweza kutambulisha bidhaa zao hivyo nipende kukushukuru Mkuu wa Mkoa Wa Dar es Salaam kwa kuungana na Wanawake hawa katika Siku yao hii Muhimu pia nikuhakikishie wakani Mimi na Wakuu wa Wilaya wenzangu tutafanya jambo kwa ajili ya kuwawezesha Wanawake hawa wajasiriamali wa Mkoa wa Dar es Salaam kujikwamua Kiuchumi."

Akiongea kwa niaba ya Vikundi vya Wajasiriamali kutoka Mkoa wa Dar es Salaam vinavyonufaika na mikopo ya asilimia 10 %ya Halmshauri mjasiriamali wa Kikundi cha wethy kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Bibi.Letisia Pius Rutta amesema "Tunaishukuru Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapindunzi na Sera mbalimbali hasa kumuinua Mwanamke Kiuchumi ameweza kutupatia mikopo na kuanzisha majukwaa mbalimbali yanayotetea haki za Wanawake hivyo tunamuahidi tutatumia fursa hii kujikwamua Kiuchumi."





# Jiji la DSM latekeleza agizo la Waziri Kairuki kwa Shule ya Kifuru, DCB yachangia madawati 30




Katika kutekeleza agizo la Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) Mhe. Angellah Kairuki wakati wa ziara yake alipotembelea Jimbo la Segerea katika shule ya Msingi Kifuru mnamo tarehe 1, Machi 2023 aliagiza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuhakikisha wanaleta madawati 500 kwa wanafunzi wa kifuru.

Hivyo Katika kutekeleza agizo hilo, leo Machi 09, 2023 Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kwa Kushirikiana na Mkurugenzi wa DCB Bank wameweza kukabidhi madawati 500 kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kifuru.

Akikabidhi Madawati hayo Mkurugenzi wa DCB Bank Ndg. Isdory Msaki ameeleza kuwa “Katika kutambua jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kukuza na kuendeleza sekta ya Elimu Nchini sisi kama DCB tumekuja na kauli mbiu isemayo ‘Elimu Mpango Mzima na Mama’ ambayo inalenga kuhamasisha suala zima la elimu nchini kwa watoto wetu hivyo tuhakikishe tunatumia vyema fursa ya elimu bure na kuwapeleka watoto wetu shuleni kupata elimu bora.”

Sambamba na hilo Ndg. Msaki amewataka wanafunzi wa Shule ya Msingi Kifuru kusoma kwa bidii kwani jamii inatambua umuhimu wa elimu na ndiyo maana Bank ya DCB imeweza kuchangia madawati kwaajili ya kuwasaidia wanafunzi hao kusoma katika mazingira bora na salama.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam Eng. Amani Mafuru amesema “Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bank ya DCB kwani Waziri wa OR-TAMISEMI alipotoa maagizo ya kuleta madawati katika Shule hii tuliongea na Mkurugenzi wa DCB na yeye kama mdau wetu aliweza kutusaidia madawati 30 ambayo leo hii tumeweza kukabidhiwa hivyo nipende kusema yote tuliyoagizwa na Mheshimiwa Waziri kuyatekeleza tutayatekeleza ipasavyo hatua kwa hatua na tumeanza na hili.”

Sambamba na hilo Eng.Mafuru amewataka wanafunzi kusoma kwa bidii kwani hayo yote yanatekelezwa ili kuwajengea wao mazingira rafiki ya kusoma na kupata elimu bora.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wanafunzi wengine Dada Mkuu wa Shule ya Msingi Kifuru Sarah Edwine amesema “Namshukuru Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutujengea madarasa, pia napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na Mkurugenzi wa Bank ya DCB kwa kutekeleza agizo la Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Kairuki na kutuletea madawati kama walivyoagizwa hivyo niwaahidi tutasoma kwa bidii na tutafaulu kwa kiwango cha juu zaidi kama mlivyotutekelezea hili na sisi tunaenda kuongeza ufaulu katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa Shule za Msingi.”



# Jiji la DSM wapatiwa mafunzo ya utekelezaji wa Mradi wa Kijana Nahodha

Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na Wataalamu wa Sekta ya Elimu na Maafisa Maendeleo ya Jamii, leo tarehe 02 Machi, 2023 wameshiriki katika kikao kazi cha uhamasishaji jamii kwa ajili ya mafunzo kupitia mradi wa Kijana Nahodha, unaotekelezwa kwa Halmashauri Tatu (3) kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Akiongea katika kikao hicho Meneja Mradi Kijana Nahodha kutoka T-MARC Ndugu Upendo Laizer ameeleza kuwa Mradi wa kijana Nahodha ni mradi uliozinduliwa na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Dtk. Hussein Mwinyi, utadumu kwa kipindi cha miaka Mitano (5) kuanzia Septemba, 2022 hadi Agosti 2026.

"Mradi huu unatekezwa na Shirika la T-MARC wakishirikiana na CARE Tanzania, Tanzania Youth Coalition (TYC), Y-LABS chini ya Shirika la Kimataifa kutoka Marekani (US AID) ambao umelenga kuwasaidia vijana kuanzia miaka 15 hadi 25 kutoka Zanzibar na Tanzania ambao walikatisha ndoto zao za masomo kwa matatizo mbalimbali."

Ameeleza Ndugu Upendo Laizer Sambamba na Hilo Mradi wa Kijana Nahodha umelenga kutekelezwa katika Mikoa miwili ambayo ni Morogoro na Dar es Salaam ambapo kwa Dar es Salaam Mradi huu utatekelezwa katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwani katika utafiti maeneo haya yameoneka kuwa na vijana wengi zaidi ambao wanaishi katika mazingira magumu na hatarishi.

Naye Meneja Mradi Kijana Nahodha kutoka Care International Ndugu Samwel Chambi ameeleza kuwa "Mradi umeandaa vikao kazi kwa lengo la kuzindua rasmi uhamasishaji jamii ili kuwatambua na kuwaandikisha vijana katika vituo vya mafunzo ya serikali ya muda mfupi yaani Open School au QT katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa vijana wenye mahitaji maalumu, mazingira magumu, yatima, pamoja na wale wanaoishi na Virusi vya UKIMWI watapatiwa ufadhili ili kuweza kutimiza adhma yao ya kupatiwa elimu na ujuzi hivyo tunategemea mchango wenu kwa kuwahamasisha wanajamii waweze kuwaandikisha vijana hao katika ofisi za Serikali za Mitaa ili waweze kupata ufadhili huo wa masomo na ujuzi kwa lengo la kupata elimu na kuendeleza ndoto zao."

Sambamba na hilo Ndugu Chambi ameeleza kuwa kutakua na zoezi la uhamasishaji ambalo litafanyika tarehe 08 na 09 Machi 2023 katika Kata zote za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa lengo la kuhamasisha zoezi hilo na kuweza kupata vijana hao.

Akiahirisha kikao hicho Mwenyekiti wa Kikao Mhe. Robert Manangwa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Huduma za Jamii Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, amesema Nipende kutoa Shukrani zangu za dhati kwa waandaaji wa mradi huu kwa kuweza kuichagua Halmashauri yetu kati ya Halmashauri tatu zilizopendekezwa Nimatumaini yangu tutaenda kuutangaza huu mradi kwa wananchi wetu na tunawaahidi ushirikiano katika kutekeleza vyema mradi huu wa Kijana Nahodha.



# Mhe Zungu akabidhi Madawati 300 shule ya Sekondari Kasulu

Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mussa Azzan Zungu tarehe 25 Machi, 2023 amekabidhi madawati 300 katika Shule ya Sekondari Ilala Kasuluiliyopo Kata ya Ilala ambapo Madawati 200 yametolewa na Mheshimiwa Zungu huku madawati 100 yakitoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa kwa kiasi kikubwa na kuhakikisha Sekta ya elimu inakua katika ufanisi na wanafunzi wote wanasoma katika mazingira bora na tulivu.

Akiongea katika hafla hiyo Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ilala Mhe. Mussa Azzan Zungu ametoa shukurani zake za pekee kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na watendaji wake wote kwa kutatua kero ya madawati katika Shule ya Sekondari Ilala Kasulu huku akiwaahidi kuendelea kushirikiana nao katika kujenga na kuimarisha sekta ya elimu nchini,

"Katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi tumeweza kutoa madawati 300 katika Shule yetu ya Sekondari Ilala Kasulu ambapo Juhudi zote hizi ni kutokana na jitihada za Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kipaumbele katika Sekta ya elimu kwani kutokana na mchango wake katika kuipa kipambele elimu kwa kujenga Madarasa Katika Shule zetu hivyo na sisi hatunabudi kuleta madawati ili wanafunzi wetu waweze kusoma katika mazingira mazuri na salama."

Aidha kwa upande wake Mwakilishi wa Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Bi.Tabu Shaibu ameeleza kuwa "Katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha mapinduzi tumeweza kutekeleza na kukuza sekta ya elimu kukua katika ufanisi unaotarajiwa hivyo ni wahakikishie changamoto hizi zitaisha kabisa kwani tutashirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha tunamaliza changamoto zote zinazokabili sekta ya elimu katika Halmashauri yetu."

Nae Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Ilala Kasulu Mwl. Hamis Ernesti Masatu amesema
"Tunamshukuru sana Mbunge wetu pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kutupatia madawati 300 ambapo kwa kiwango chake tumepunguza idadi ya uhitaji wa madawati katika shule hii ya Sekondari Ilala Kasulu kwani tumepata nyongeza ya madawati takribani 86 hivyo wanafunzi wetu wataweza kusoma katika mazingira tulivu na idadi ya ufaulu itazidi kuongezeka.

Pia tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya miaka hii miwili ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu tuliweza kupata fedha za madarasa ya Uviko ila kutokana na ufinyu wa eneo fedha hizo zikahamishiwa sehemu nyingine".





# DC Ilala Ashiriki zoezi la usafi huku akiyataka Makampuni yaliyoko maeneo ya barabarani kupanda miti na kufanya usafi

Katika kuendeleza na kutekeleza kampeni ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla, Mkuu wa Wilaya ya Ilala Leo Machi 25,2023 ameshiriki zoezi la usafi katika Kata ya Kipawa, ambao usafi huo ulijumuisha maeneo ya Barabara ya Air Port, Maeneo ya Kata ya Kiwalani, Vingunguti na Minazi Mirefu hadi kufika daraja la Mfugale.

Zoezi hilo lililoongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo akiambatana na Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala , Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Diwani wa Kata ya Kipawa , Diwani wa Viti Maalumu, Watumishi Kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Watendaji wa Mtaa, viongozi wa Chama cha Mapinduzi ,viongozi kutoka shujaa wa maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA),wadau kutoka Bank ya CRDB na NMB, wadau mbali mbali wa usafi wakiwemo Wejisa Company limited , Kajenjere Trading Company Limited, Sateki Trading Limited, pamoja na Wananchi wa Kata ya Kiwalani,Minazi Mirefu Kipawa na Vingunguti.

Akiongoza Mhe. Edward Mpogolo amewashukuru viongozi wa Serikali za mitaa na Kata kwa kushiriki kikamilifu katika zoezi la usafi wa mwisho wa mwezi huu kwani wameonesha kuwiwa na jambo hili.

“Kutokana na ukubwa wa Barabara ya Airport napenda kuwaomba watu wa maduka na Makampuni yaliyoko barabarani waboreshe maeneo Yao huku upande wa katika ya barabara tutahakikisha Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tunashirikiana na wadau mbali mbali ili kuhakikisha barabara hii inakuaje safi na bora kwani Dar es Salaam hususani Wilaya ya Ilala Ndio Kitovu cha kupokea wageni wanaoingia Nchini kwani hivi karibuni tutakua na ugeni mkubwa Nchini kwetu ambapo tutampokea Makamu wa Rais wa Marekani Mhe. Kamala Harris hivyo tuweke mazingira yetu katika hali ya usafi wakati wote ili pindi wageni wetu hao wanapofika wajivunie mazingira ya Nchi yetu yanavyopendeza na kuvutia yakiwa katika hali ya usafi .”

Sambamba na hilo Mhe. Mpogolo amemuelekeza Mkurugenzi wa Jiji kwa kushirikiana na watendaji wake kuhakikisha wanaenda barua na kuwapelekea wafanyabiashara wote wenye Majengo kuanzia barabara ya Airport hadi Ikulu ili kuona namna gani watawaelekeza kuboresha mazingira na miti gani waweze kupanda kwenye maeneo Yao ili kuboresha mazingira ya Mji wetu.

Aidha Mhe. Mpogolo amewataka watu wa viwanda na makampuni yaliyoko barabarani kuhakikisha wanafanya usafi mara kwa mara katika maeneo yao na kupanda miti inayokubalika.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam Bi.Tabu Shaibu ameeleza kuwa kampeni hii ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam imekua ya mafanikio zaidi kwa Jiji la Dar es Salaam kuwa Safi kwani wananchi wameonekana kujitokeza kwa wingi katika zoezi la usafi.

“Nipende kutoa Shukrani zangu za dhati kwa Mkuu wa Mkoa Wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla kwa kuanzisha Kampeni hii ambayo ni endelevu hivyo niwaombe wananchi kuhakikisha usafi ni Sehemu ya maisha yetu ya Kila siku na si mpaka tusubiri usafi wa mwisho wa mwezi.” Ameeleza Bi. Tabu Shaibu.

# Wazazi na Walezi watakiwa kuwapa Watoto Mlo Kamili



Wazazi na Walezi wametakiwa kuhakikisha watoto wanapata mlo kamili wenye virutubisho vyote muhimu vya makundi ya chakula kwa ajili ya ukuaji wa binadam ikiwemo protini, wanga, vitamini, madini, mboga mboga, matunda na maji.

Hayo yamebainishwa leo tarehe 29 Machi, 2023 na Afisa Lishe Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Bi. Neema Mwakasege wakati wa zoezi la utoaji wa Elimu kwa vitendo juu ya masuala ya lishe, lililoendeshwa katika Kata ya Mnyamani ambapo amewasisitiza wazazi na walezi kuhakikisha watoto hawakosi mlo wenye makundi yote ya chakula ili kuwakinga na maradhi sambamba na kuwakinga dhidi ya udumavu.

"Wapeni watoto chakula chenye mjumuisho wa makundi yote muhimu katika kila mlo, Maji hayamo katika makundi hayo lakini msiache kuwapa maana maji ndio sehemu kubwa katika mwili wa binadamu na ndio yanayosaidia makundi yote hayo yaweze kufanya kazi kwa urahisi mwilini. Vilevile nisisitize kula mbogamboga kwa wingi kwani husaidia kuongeza damu mwilini." Alisema Bi. Mwakasege.

Nae Bi. Sophia Elias, Afisa Ustawi wa Jamii kutoka Kituo cha Afya Buguruni amewaomba wazazi na walezi kuacha tabia ya kukatisha kuwapeleka watoto kliniki pindi wanapofikisha miaka miwili na nusu hasa baada ya kumaliza chanjo zilizozoeleka ikiwemo ile ya ugonjwa wa Surua, mlango wa kizazi, kupooza, homa ya Uti wa Mgongo na ile ya kujikinga dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu.

Aidha, Afisa Mtendaji wa Kata ya Mnyamani Ndg. Javari Mrisho alilisitiza suala la Ukatili wa Kijinsia unaofanyika majumbani na kuwaasa wananchi kutoa taarifa haraka pindi wapatapo taarifa za matukio hayo. "Wananchi msiwe waoga kutoa taarifa. Watu wanafanyiwa ukatili lakini kwa uoga hawatoi taarifa kwenye vyombo husika. Nawaasa nikiwa kama Mtendaji wa Kata kama ni wewe unafanyiwa ukatili au una taarifa za mtu yoyote anaefanya au kufanyiwa ukatili wa kijinsia basi utoe taarifa mara moja." Amesema Ndg. Mrisho

# Idara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara wafanya mafunzo ya namna ya Utendaji kazi katika Idara hiyo Mpya







Tarehe Iliyowekwa: March 29th, 2023
Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia Idara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara leo Machi 29,2023 wameanza rasmi mafunzo ya kujifunza namna ya utendaji kazi ikiwa idara hiyo ni mpya. Mafunzo hayo yanayofanyika katika Ukumbi wa Karimjee Jijini Dar es Salaam yatawezeshwa kwa siku 10 na wawezeshaji mbalimbali kutoka Wizara ya Uwekezaji,Viwanda na Biashara, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMi), Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), pamoja na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Akifungua Mafunzo hayo kwa niaba ya Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Bi. Tabu Shaibu amewataka watumishi kutoka Idara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuhakikisha wanakua makini kusikiliza yote watakayoelekezwa katika mafunzo hayonili kuweza kufikia lengo lililokusudiwa.

Aidha Bi.Tabu Shaibu ameweza kumshukuru Rais Wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuanzaisha wizara mpya ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambayo italeta tija katika kukuza sekta ya Viwanda na biashara nchini. "Nipende kutoa Shukrani zangu za dhati kwa Rais wetu kwa kuanzisha wizara mpya ya Uwekezaji ,Viwanda na Biashara pia niwashukuru wawezeshaji wote mlioungana na Watumishi wetu kutoka Jiji la Dar es Salaam kujitolea kuja kuwapa mafunzo haya ambayo yatakua na manufaa makubwa kwa Idara yetu kupanga mikakati mathubuti ya namna ya kuendesha biashara zetu na kuweza kukuza mapato ya Halmashauri kwa kiwango cha juu zaidi hivyo niwaombee msikilize kwa makini na nimatumaini yangu baada ya mafunzo haya mtakua mmefikia lengo lililokusudiwa".

Vilevile Bi.Tabu Shaibu alitoa wito kwa Watumishi wa Idara ya Uwekezaji,Viwanda na Biashara kuhakikisha ndani ya siku kumi za mafunzo wahakikishe wamepata walichokikusudia pia wakimaliza kazi wafanye kazi kwa kushirikiana ili kuweza kupata mafanikio ya pamoja katika kuongeza mapato ya Halmashauri ya Jiji na Nchi kwa ujumla wake.

Kwa Upande wake Afisa Biashara Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Bw.Amos Jeremiah ameeleza kuwa "Sisi kama watendaji wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara tumeungana na wenzetu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuhakikisha tunawapa muongozo na uelewa wa namna ya utendaji kazi katika Idara mpya ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha majukumu ya kazi yanatekelezwa kwa kiwango cha juu zaidi."
Naye Mwezeshaji kutoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Bw. Ishara Nzamilisi ameeleza kuwa kwa kushirikiana na Wadau kutoka BRELA na TANTRADE ni matumaini yao mafunzo haya yataenda

# Miaka miwili ya Rais Samia yanufaisha Wavuvi wa Soko la Kimataifa la Samaki Feri




Tarehe Iliyowekwa: March 22nd, 2023
Katika kuadhimisha miaka miwili ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan Leo Machi 22, 2022 Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Soko la Kimataifa la Samaki Feri wameandaa hafla maalumu ya kumpongeza na kumuunga Mkono Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka miwili ya utawala wake.

Akitoa shukrani zake za dhati kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na bodi nzima ya Soko la Kimataifa la Samaki Feri mgeni rasmi ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Mussa Azzan Zungu amesema "Shughuli hii sio ndogo kwa Taifa letu kwani Hafla hii ya kumpongeza Rais wetu imefanyika bila upendeleo ukilinganisha na mambo aliyofanya katika kipindi hiki cha miaka miwili ya uongozi wake hata hivyo amekua akiwajali sana wavuvi kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwani ameweza kutoa fedha takribani bilioni 200 kwa ajili ya kujenga Bandari ya Uvuvi Mtwara huku Milioni 37 ikitolewa kwaajili ya kununulia boti la kusaidia shughuli za ulinzi wa rasilimali za Uvuvi, Doria na uokozi katika maeneo ya fukweza."

Sambamba na hilo Mhe. Zungu amewataka wadau wa uvuvi wote kushirikiana pamoja kupiga vita uvuvi haramu kwani huleta madhara makubwa kwenye afya za wananchi na pia uharibifu wa Mazingira.

Akisoma taarifa fupi ya Mafanikio ya Soko la Kimataifa la Samaki Feri Meneja wa Soko hilo Bw. Denis Mrema ameeleza kuwa "Mafanikio ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan yanaonekana katika kila sekta ya Huduma za Jamii, Uchumi, Miundombinu, Elimu ,Uvuvi na Siasa kwani kwa upande wa Soko Kimataifa la Samaki feri tumeweza kufanikiwa kupitia ubunifu wa Rais wetu wa kuanzisha filamu ya 'Royal Tour' soko letu katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake tumeona mabadiliko makubwa kwa kuweza kupata watalii kutoka ndani na nje ya Tanzania wakitembelea soko letu." Alisema Bw. Mrema

Aidha Bw. Mrema ameendelea kusema "Katika kipindi cha miaka miwili ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wananchi wameweza kunufaika na mikopo ya Uvuvi kwa kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kupata mikopo ya zana za Uvuvi hivyo kupitia mikopo hiyo wavuvi hao wameweza kuinua kipato chao na kuimarisha utendaji wa shughuli zao."



Naibu spika wa Bunge la jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Mussa Azzan Zungu



# BARAZA LA MADIWANI WA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM , LAPITISHA HERIA NDOGO

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam limefanya kikao cha kupitia na kupitisha sheria ndogo za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam leo Machi 6, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Arnatoglou, Jijini Dar es Salaam, lengo likiwa ni kufanyia marekebesho madogo ya sheria za awali katika maeneo ya ushuru wa Masoko, tozo za fremu za maduka pamoja na ada ya ulinzi shirikishi.

Akiongea katika kikao hichokikao Naibu Meya wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Mhe. Ojambi Massaburi ambaye aliongoza Kikao kwa Niaba ya Mstahiki Meya, amesema kanuni inaeleza vizuri kwani lengo sisi ni kupitia sheria hizi na kuzifanyia marekebisho lengo likiwa ni kutomuumiza mwananchi yoyote wala kumpendelea mtu yoyote kwani sheria hizi zinadumu kwa muda mrefu hivyo tuzifate na kuzisimamia.

Wakijadili marekebishio ya sheria hizo kabla ya kuzipitisha baraza la Madiwani limeridhia kuwa kwa upande wa ushuru wa masoko tozo zitengwe kulingana na eneo Soko lilipo kwani masoko ya pembezoni mwa mji hawawezi kukidhi mahitaji ya kulipia fremu za Masoko kama Masoko ya mjini.

Adhia Vikundi vya Ulinzi Shirikishi kuanzia ngazi ya Mtaa ambapo Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa ndiye msimamizi wa zoezi hilo na katika ngazi ya Kata Mtendaji wa Kata ndiye msimamizi wa Kata husika.

# Zoezi la upandaji Miti laendelea kwa Kasi Wilaya ya Ilala



Katika kuelekea siku ya upandaji miti Kitaifa ambayo hufanyika kila tarehe 1 Aprili Wilaya ya Ilala leo tarehe 31, Machi 2023 wameadhimisha siku ya upandaji miti kwa ngazi ya Wilaya ambapo miti 300 imeweza kupandwa katika Shule ya Msingi Muungano iliyopo Kata ya Kiwalani Jiji la Dar es Saalam.

Akiongoza zoezi hilo la upandaji miti kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala Bi.Charangwa Selemani amesema "Kutokana na mabadiliko ya tabia ya Nchi inatupasa tupande miti kwa wingi ili kukabiliana na changamoto hii hivyo sisi kama Wilaya ya Ilala tumeweza kupanda miti elfu 11 na leo hii katika maadhimisho haya ya siku ya upandaji miti ngazi ya Wilaya tumeweza kupanda miti 300 katika Shule ya Msingi Muungano huku miti hiyo ikiwa ni miti ya matunda kama Miembe, Michungwa, Mipera, Mikungumanga pamoja na miti ya Kivuli hivyo nitoe wito kwa Waalimu na Wanafunzi kuhakikisha miti hii inatunzwa vizuri ili iweze kukua kwa wakati na tutakuja kukagua kuona kama mnatekeleza haya".

Sambamba na hilo Bi.Charangwa ametoa wito kwa Wananchi wote kuhakikisha wanapanda miti kwa wingi katika maeneo yao ya makazi lengo likiwa ni kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi. " Kulingana na kauli mbiu ya siku ya upandaji miti kitaifa isemayo 'Miti ni Afya' pamoja na kutekeleza maagizo ya Makamu wa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kila Wilaya kuhakikisha wanapanda miti Milioni 1.5 kila Mwaka natoa wito kwa wananchi wote wa Wilaya ya Ilala kuhakikisha mnapanda miti kwenye makazi yenu ili tuweze kufikia lengo letu hivyo sisi kama Wilaya tutaendelea kushirikia na Wadau mbalimbali kuhakikisha tunapanda miti kwa Wingi hasa maeneo ya hifadhi ya mito pamoja na maeneo ya pembezoni mwa barabara".

Akiongea kwa niaba ya Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Afisa Elimu Msingi Bi.Siporah Tenga ameeleza kuwa katika kutekeleza kampeni ya soma na Mti wanafunzi kila mwanzafunzi atatakiwa kupanda mti wake na kuhakikisha anautunza vyema, "Sisi kama viongozi tutahakikisha tunasimamia vyema zoezi hilo na kwa ukaribu zaidi kuhakikisha miti hii inayopandwa inatuzwa vyema na kuangaliwa kwa ukaribu zaidi ili iweze kukua kama ilivyotarajiwa."
Naye Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa mazingira wa Halmasahuri ya Jiji la Dar es Salaam Bi. Theresia Denis ameeleza kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 ya kuendeleza programu mbalimbali za upandaji miti na ufugaji nyuki ili kutunza mazingira..



## HALMASHAURI KUU CCM ( W) ILALA WAPONGEZA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CCM KWA MIRADI YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

Katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 hadi 2025 leo Machi 16,2023 Halmashauri kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ilala wamefanya Mkutano wa kujadili utekelezaji wa miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuanzia Januari 2021 hadi Disemba 2022.

Mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa Arnatouglou Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam na uliweza kuhudhuriwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Ilala, Katibu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Ilala, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ilala, Wajumbe wa Halmashauri kuu Wilaya ya Ilala pamoja na Watumishi kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza katika Mkutano huo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Ilala Ndg. Said Sidde amesema "Niwapongeze Wajumbe wa Halmashauri kuu kwa kupokea na kupitisha Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) pia nipende kuipongeza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kutekeleza Ilani ya chama kwani wameweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuboresha huduma za wananchi ila niwaombe viongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuhakikisha mnatekeleza yale yote tuliyowaelekeza wakati wa ziara yetu na pia muhakikishe miradi yote inatekelezwa kwa wakati uliopangwa".

Kwa upande wake Naibu Spika wa Bunge ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ilala Mhe. Mussa Azzan Zungu amesema "Nawashukuru sana wilaya ya Ilala kwa kuwa Wahamasishaji wazuri kwani Kata zote 36 zimeweza kupata hamasa juu ya utekelezaji wa Ilani ya chama cha Mapinduzi, mmelifurahisha Taifa pamoja na Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kwani mmekua mkitekeleza majukumu ya Kamati Kuu hadi kuwadhamini wajumbe wa shirika".

Akiwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala Bi. Charangwa Selemani ameeleza kuwa "Katika kutekeleza ilani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Idara zake zikiwemo Idara ya Elimu, Idara ya Afya, Idara ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Idara ya Maliasili na Mazingira ambapo katika Idara ya Elimu Msingi na Sekondari Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeendelea kupokea Fedha kwa ajili ya kuboresha Elimu ya Msingi ambapo asilimia 40% ya fedha hizo zinanunulia vitabu, huku fedha zinazopokelewa shuleni ni asilimia 60% ambapo asilimia 30% inanunua vifaa vya kufundishia ambavyo siyo vitabu, asilimia 30% hutumika katika ukarabati wa miundombinu huku asilia 20 % zikitumika kwenye mitihani, asilimia 10% zikitumika kwa ajili ya UMITASHUMTA na 10% Utawala. Pia kwa upande wa kuboresha Elimu ya Sekondari tuliweza kupokea shilingi bilioni 5.1 kwa mwaka 2021 zikiwa ni fedha za Uviko 19 ambazo zilitumika kujenga madarasa 255 na yote yalikua madarasa ya msambao huku mwaka 2022 Halmashauri ilipokea kiasi cha shilingi bilion 6.2 kutoka Pochi la Mama ambazo zilitumika kujenga madarasa 310 huku 37 yakiwa ya ghorofa".

Kwa upande wa kuboresha huduma za Afya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeendelea kutoa huduma mbalimbali za afya kupitia vituo vyake vya Afya huku elimu ya afya ikiendelea kutolewa kwa Wananchi.

Aidha Bi. Charangwa ameendelea kusema Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii imefanya uhamasishaji wa kutoa mikopo kwa Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu kwa pesa za asili 10% za mapato ya ndani ya Halmashauri ambapo kiasi cha shilingi bilioni 3.6 zilitolewa kwa vikundi 316 vya vijana huku idara ikiendelea kutoa elimu ya ujasiriamali , elimu rika ,




Umoja wa Wajasiriamali Walemavu Mkoa wa Dar es Salaam (UWAWADA) leo Machi 17, 2023 wamefanya kongamano la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza miaka miwili ya uongozi wake na kumshukuru kwa kuendelea kusisitiza mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri ambayo watu wenye ulemavu ni wanufaika.

Akizungumza kwenye kongamano hilo lililofanyika kwenye Viwanja vya Karume kwa niaba ya Mkuuwa Mkoa wa Dar es Salaam, Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala Bi. Charangwa Selemani alitoa pongezi kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza Miradi yote iliyoachwa na Hayati John Pombe Magufuli kwa kasi na ubora uleule, na kumshukuru kwa kuendelea kusisitiza mikopo inayotolewa kwa watu wenye ulemavu kwani huwasaidia kuwainua kiuchumi.

Aidha Bi. Charangwa amewapongeza Umoja wa Wajasiriamali Walemavu Dar es Salaam (UWAWADA) "Niwapongeze kwa kuandaa shughuli nzuri yenye lengo zuri la kumpongeza mama yetu, mnaonesha jinsi gani mna shukurani maana kila mtu angeweza kukaa peke yake na kushukuru, hivyo mtaenda kumtia Mhe. Rais" Amesema Bi. Charangwa.

Nae Ndg. Juma Malecha ambae ni Mwenyekiti wa Umoja huo amesema wanashukuru Uongozi bora wa Serikali ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwani ndani ya miaka miwili ya uongozi wake aliweza kukutana na Watu wenye Ulemavu na kusikiliza changamoto zao, Pia Mhe. Rais ameendelea kusisitiza suala la mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri huku kundi hilo likiwa miongoni mwa makundi yaliyonufaika na mikopo hiyo kwa asilimia 2. Aliongeza kwa kusema kuwa ndani miaka miwili hiyo Mhe. Dkt. Samia ameweza kufufua Vyuo vya Ufundi kwa Watu wenye Ulemavu ambavyo vilikuwa vimefungwa ambapo katika vyuo hivyo wanapata chakula na malazi bure na pia amekemea unyanyapaa.



# FAIDA ZA MFUMO WA TAUSI KWA KUZINGATIA MAHITAJI YA WADAU NA KASI YA UKUAJI WA SAYANSI NA TEKINOLOJIA

SELF SERVICE(KUJIHUDUMIA): MFUMO WA TAUSI UMELENGA KUMSAIDIA MTEJA AWEZE KUJIHUDUMIA MWENYEWE KUPITIA DIRISHA LA MTEJA AU TAXPAYER PORTAL.
MTEJA ATAWEZA KULIPA TOZO, USHURU,LESSENI, FAINI AU VIBALI MBALIMBALI PASIPO KWENDA OFISI ZA MAPATO ZA HALMASHAURI.

CASHLESS ACROSS THE GLOBE(BILA FEDHA DUNIANI KOTE ):
HII HUMSAIDIA MTEJA AWEZE KUFANYA MALIPO MBALIMBALI KWA KUTUMIA VISA, MASTERCARD, NA NAMBA YA MALIPO KUTOKA MFUMO WA MALIPO WA KIELEKTRONIKI WA SERIKALI (GEPG)

TAUSI